



THE  
LUTHERAN  
WORLD  
FEDERATION

A Communion  
of Churches

[lutheranworld.org](http://lutheranworld.org)

## UJUMBE WA PASAKA: MUDA WA KUFIKIRI JUU YA MITAZAMO MIPYA

### Makamu wa Raisi, FMKD, Desri Maria Sumbayak, Kanisa la Kikristo la Indonesia

Kwangu mimi binafsi, kipindi cha Pasaka cha mwaka huu ni cha tofauti kabisa. Siku mbili kabla ya Ijumaa Kuu wananchi wote wa Indonesia tutakuwa tunaipa demokrasia nafasi kubwa kwa kutimiza haki yetu ya msingi ya kupiga kura wakati wa uchaguzi mkuu. Ninaamini kuwa uchaguzi wa mwaka huu utakuwa na mchango mkubwa katika mstakabali wa maisha ya demokrasia ya nchi yetu katika siku za baadaye.

Kila siku, katika mwaka huu, tumepitishwa kwenye kitu kinachoitwa, "kampeni chafu," ambacho ni muunganiko wa habari zisizo za kweli na hotuba za chuki zinazosambazwa kwa njia ya mitandao ya kijamii. Vita imeanza kati ya wafuasi wa makundi mawili yenye ushindani mkubwa wa nafasi ya uraisi, ambapo ningeweza kuvielezea kuwa ni vita kati ya chama cha kitaifa cha kisiasa na chama cha kisiasa cha kidini, hali inayoleta wasiwasi kwenye vitongoji na pia kuleta ufa kati ya makundi ya kikabila na kidini.

Wakati huo huo uchaguzi upo katika kipindi ambacho Wakristo wanajiandaa kukumbuka kifo na ufufuo wa Yesu Kristo. Mimi mwenyewe najiandaa kuona upendo wa Mungu kwetu katika hali hii ngumu ya kisiasa.

Ni ukweli usiopingika kuwa katika kipindi hiki cha kampeni za uchaguzi zinazoendelea hapa Indonesia, Wakristo wengi wanaona wameingia katika mtego wa hasira na kuchanganyikiwa. Tunapotaka kukuza amani na haki, tunachekwa na kuitwa wanafiki, waoga na wasio na imani ya kweli. Hali hii ya kisiasa imeleta pia ufa kati ya Wakristo. Ni kweli, kwa upande wa Asia, na hasa Mashariki ya Kati, tunaona washirika wa Kanisa wakiwa katika hali zinazofanana, wakimlilia Mungu alete amani na haki.

Tutawezaje kuona sadaka ya Yesu katika vita vya kisiasa? Kifo cha Yesu ni kifo cha mapambano na maumivu. Sadaka yake inahusha maisha yetu. *Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita tazama! Yamekuwa mapya* (2 Wakorintho 5:17). Wakati wa Jumapili ya Pasaka, kila wakati tunakumbuka damu ya Yesu na sadaka, tunakumbuka kuwa sisi ni viumbe vipya. Nafsi zetu zilizochoka zinachangamshwa na neema yake. Mitazamo yetu ya kizamani inafanywa mipya kwa upendo wake. Mungu haahidi ulimwengu mpya au kweli mpya. Bali, Mungu anatupa sisi mtazamo mpya wa kuona ukweli.

Ni maombi yangu kuwa katikati ya hali ya kisiasa na zingine zinazofanana na kugubikwa na wasiwasi na mivutano, ujumbe wa Pasaka wenye matumaini na ukweli mpya ulio katika Yesu Kristo utatusaidia kuonya hali ya mioyo iliyovunjika miongoni mwetu.

*Bi Desri Maria Sumbayak ni Makamu wa Raisi Fungamano la Makenisa ya Kilutheri Duniani (FMKD) eneo la Asia. Ni mshirika wa Kanisa la Kikristo la Indonesia.*